

UJUMBE KWA WAZAZI NA WANAFUNZI

Yahusu: COVID-19 – Sherehe na Matukio ya Mahafali Katika Sura Mpya

Wapendwa wanafunzi na wazazi:

Kwa wahitimu, suala la kufungwa shule lililosababishwa na ugonjwa tandavu wa COVID-19 linavuruga shughuli za mahafali. Wengi wao wanajiuliza jinsi mafanikio yao ya kitaaluma yatakavyoadhimishwa.

Kamati ya kanda, ambayo inaundwa na wakuu watano wa shule, walimu wanne, wanafunzi wanne, na mwakilishi wa Idara ya Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto, ilijadili njia za kuadhimisha mafanikio haya ya wahitimu, hatua za kulinda Afya ya Umma zinazohusiana na COVID-19 zikizingatiwa.

Baada ya kuchanganua vikwanzo husika na mambo muhimu yaliyobainishwa na wanafunzi, kamati ilikubaliana kwamba itakuwa vigumu sana kukidhi uhalisia wa kila shule kutokana na kutofautiana kwa idadi ya wahitimu. Kwa hiyo kamati ilijadili matukio kadhaa yanayoweza kufanyika kwa ajili ya sherehe za mahafali na dansi ya uhitimu, na ikakubaliana kwamba itakuwa vyema kwa kila shule kuandaa mpango wake binafsi mahalia.

Moja ya matukio yaliyopendekezwa yanajumuisha kipengele cha kanda kwa njia ya mtandao na kipengele mahalia (mtandaoni au ana kwa ana) ili shule ziweze kubuni sherehe zao za mahafali wao binafsi, huku zikizingatia hatua za kulinda Afya ya Umma.

Suala la kuahirisha matukio haya mpaka taraha ya hapo mbeleni halipendekezwi ikizingatiwa muda unaoweza kupita kabla mikusanyiko kuruhusiwa tena. Hata hivyo, shule zinaweza kuchagua kuunga mkono mipango ya siku za usoni ya wanafunzi kama wakipenda kufanya hivyo.

Huku wakishauriana na wanafunzi na wafanyakazi, wakuu wa shule kwa sasa wanafanya kazi ya kuandaa mpango kwa ajili ya shule zao. Mpango huo, ambao utaidhinishwa ifikapo Mei 26, 2020, utalazimika kuzingatia hatua za kulinda Afya ya Umma. Ni dhahiri sherehe hizi hazitafanana na zile zilizofanyika hapo nyuma, lakini kamati inaamini itawezekana kuyatambua mafanikio ya wanafunzi kwa njia maalum na ya kipekee.

Tunatambua kwamba suala hili ni muhimu sana kwa wahitimu. Ni hatua kubwa ya kimaisha ambayo inastahili kuadhimishwa kwa namna ya kipekee.

Mkuu wa shule yako awatashirikisha mpango husika hivi karibuni.